Kuboresha Uzingatiaji wa Kulipa Kodi Tanzania

Maoni ya walipa kodi

Sikika

Sikika 2022

Kuboresha Uzingatiaji wa Kulipa Kodi Tanzania

Maoni ya walipa kodi

Utafiti kuhusu Vichocheo vya Ulipaji kodi wa Hiari katika Ngazi ya Serikali za Mitaa

Utafiti huu umefadhiliwa na Programu ya
Utawala Bora wa Fedha (GFG)

Inayotekelezwa na

giz Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit (GIZ) GmbH

Kwa niaba ya

german cooperation
DEUTSCHE ZUSAMMENARBEIT

Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Swiss Agency for Development and Cooperation SDC

Co-funded by the European Union

Yaliyomo

Orodha ua Vifupisho v
Shukrani vi
Muhtasari vii

Utangulizi 1
- Vihatarishi vya Ulipaji Kodi 1
- Vichocheo vya Ulipaji Kodi 2
- Tatizo la Kiutafiti 2
- Malengo ya Utafiti 3

Mbinu za Utafiti 3
- Fieldwork 3
- Analysis 4

Utafiti 5
- Makundi ya walipa kodi 5
- Majukumu ya mlipa kodi 6
  - Usajili wa Mlipa kodi 6
  - Utunzaji wa Kumbukumbu 6
  - Ulipaji kodi kwa wakati 6
  - Ufuatiliaji wa vihatarishi vya ulipaji kodi 6
- Vihatarishi vya Ulipaji Kodi 7
  - Uandikishaji Walipa kodi 7
  - Utunzaji wa Kumbukumbu 6
  - Malipo kwa Wakati 6
  - Mpangilio wa Vihatarishi vya Ulipaji Kodi 9
- Vichocheo vya Ulipaji Kodi 10
  - Jinsi ya kushughulika na wakwepa kodi 10
  - Jinsi ya kuwahudumiwa Walipa Kodi 10
  - Taarifa na Elimu ya Kodi 11
  - Mzigo wa Kulipa Kodi 13
  - Faida za Kulipa Kodi 14
  - Utamaduni wa Kulipa Kodi 15
  - Mpangilio wa Vichocheo vya Ulipaji Kodi 15
  - Uchambuzi wa Jinsia 16

Majadiliano 17
- Vihatarishi vyaUlipaji kodi 17
- Vichocheo vya Ulipaji Kodi 17
- Tathmnini na Ufuatiliaji wa Mikakati ya Vihatarishi vya Ulipaji Kodi 18

Hitimisho na Mapendekezo 19

Orodha ya Rejea 22

Orodha ya Vifupisho

CAG	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali
CC	Halmashauri ya Jiji
DC	Halmshauri ya Wilaya
EFD	Mashine za Kodi za Kielektroniki
LGA	Mamlaka ya Serikali za Mitaa
MC	Manispaa
MSME	Biashara ndogondogo, Ndogo na za Kati
S/N	Nambari ya Ufuatiliaji
TC	Halmashauri ya Mji
TFS	Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania
TIN	Nambari ya Utambulisho wa Mlipa kodi
TRA	Mamlakaa ya Mapato Tanzania
TZS	Shilingi za Tanzania

Acknowledgements

Utafiti huu kuhusu vichocheo vya ulipaji kodi kwa hiari umewezekana kutokana na michango ya watu wengi binafsi na mashirika.

Tunashukuru kwa msaada wa kiufundi na kifedha tuliopokea kutoka kwa Shirika la Maeandeleo la Ujerumani (GIZ) kupitia Programu ya Utawala Bora na Kifedha, na shukrani za pekee ziende kwa Vanja Ćurčic, ambaye alisimamia utafiti huo.

Tunashukuru kwa msaada tuliopata kutoka kwa Silas Samaluku na Linus Kahendaguza kutoka Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Walitambulisha shughuli za utafiti kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa na kutoa ushirikiano kwa timu ya utafiti ya Sikika.

Tunaishukuru timu ya watafiti ikiwa ni pamoja na washauri Aisha Hamisi na Revocatus Wambura na wafanyakazi wa Sikika, Godfrey Mfumu na Alphonce Chuwa, ambao walikusanya, kutafsiri na kunakili takwimu kutoka mamlaka nane za Serikali za Mitaa katika mikoa minane tofauti.

Kutoka Sikika, tunathamini pia kazi iliyofanywa na Florian Schweitzer ambaye alisimamia utayarishaji na utekelezaji wa utafiti, kuchambua takwimu zilizokusanywa na kutoa muhtasari wa ripoti hii.
Pia tunamshukuru Alice Monyo, ambaye alitoa maoni muhimu wakati wa mchakato wa kuandika ripoti hii. Tunatambua pia mchango wa Lilian R. Kallaghe ambaye alitafsiri ripoti hii kutoka kwenye Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili.

Kwenu nyote tunasema, ahsanteni sana.

Irenei Kiria,
Mkurugenzi Mtendaji wa Sikika

Muhtasari

Katika kipindi cha miaka iliyopita, Serikali ya Tanzania imekuwa ikichukua hatua kadhaa za kifedha na kiutawala ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani. Katika jitihada hizo, Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) pia zinatakiwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato yao kutokana na vyanzo vya ndani. Hata hivyo, mchakato huo umekuwa na changamoto ya muda mrefu kutokana na vikwazo vya uwezo kwa upande wa utawala na pia kutokana na kutozingatiwa na walipa kodi. Vihatarishi vya ulipaji kodi huanzia kwenye mchakato mzima wa usimamizi wa mapato, kuanzia usajili wa walipa kodi, uzingatiaji wao wa jukumu la kuweka kumbukumbu, na ulipaji wa madeni ya kodi, kwa wakati.

Kujaribu kukomesha tabia (dalili ya kutofuata sheria) kwa kuweka vikwazo vikali kwa wakwepa kodi kunaweza kuwa na athari za muda, lakini pia kunaweza kuleta hisia za chuki dhidi ya mfumo wa kodi na kusababisha kutofuatwa kwa sheria. Hivyo, mkakati endelevu wa ukusanyaji wa mapato unahitaji kuchunguza msingi wa vichocheo vya uzingatiaji na kushughulikia chanzo chake (na sio dalili) ya kutofuata sheria. Kwa sababu hizo, Sikika ilifanya utafiti wa kubaini vichocheo vya ufuasi wa ulipaji kodi kwa hiari ambavyo vinawazuia au kuwakatisha tamaa walipakodi wa ndani kutekeleza majukumu yao na kutoa mapendekezo ya jinsi mamlaka za mapato ya serikali za mitaa zinavyoweza kubuni mikakati madhubuti ya utatuzi ili kukuza uzingatiaji wa kodi na kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato.

Mbinu zilizotumika

Utafiti huu ulifanyika kati ya Januari na Februari 2022 na ulijumuisha Mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGAs) kutoka mikoa minane yenye uwiano wa kijiografia. Katika hatua ya awali, vikao vya mashauriano vilifanyika kwa kila uongozi wa mapato ndani ya Serikali za Mitaa ili kubaini vyanzo vyenye uwezekano mkubwa wa mapato yasiyokusanywa, ili kubainisha sheria ndogo zinazoelekeza wajibu wa mlipakodi, na kuchagua sehemu ya walipa kodi ambayo inapaswa kushiriki katika majadiliano ya vikundi. Hatua ya pili, mijadala 24 ya vikundi lengwa ilifanyika (3 katika kila Halmashauri 8) na washiriki wapatao 8-10. Vikundi vilivyolengwa vilijadili maswali ya wazi ili kuchunguza a) changamoto za washiriki wakati wa usimamizi wa mapato, b) vichocheo vya msingi vya mwenendo wa uzingatiaji, na c) kutoa mapendekezo ya jinsi idara za ukusanyaji wa mapato za Halmashauri zinavyoweza kuimarisha uzingatiaji wa taratibu za ulipaji kwa hiari.

Vihatarishi vya Ulipaji Kodi

Walipoulizwa kuhusu changamoto walizopitia wakati wa mchakato wa **usajili wa walipakodi**, nusu ya wanakikundi hao 24 walitaja muda wanaotumia kuzifikia mamlaka mbalimbali za serikali. Robo ya wanavikundi walipendekeza menejimenti ya mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kuanzisha vituo vya kutolea huduma zote kwenye sehemu moja, theluthi moja ilipendekeza menejimenti za mapato kuwatembelea na kusajili walipakodi katika maeneo yao ya biashara, na 38% ilipendekeza kupunguzwa kwa gharama za usajili wa walipa kodi.

Walipakodi wana wajibu wa **kuweka rekodi** ili kuruhusu wasimamizi wa mapato kubainisha wajibu wa kodi. Ingawa Kanuni za Ushuru wa Mapato (2012) zinataka kwamba Mashine za Kielektroniki za Kulipia Kodi (EFD) zitoe chapisho ambalo hudumu kwa muda usiopungua miaka mitano, karibu nusu ya makundi lengwa na walipa kodi walisema kuwa risiti za fedha zilizochapishwa na mashine hizo zinafifia na hazisomeki baada ya siku kadhaa.

Mara kwa mara, walipakodi pia hukabiliwa na gharama za ufuatiliaji wanapotembelea ofisi mbalimbali za serikali za mitaa, ambazo nyingi ziko mbali ili kupata nambari ya udhibiti wa malipo na kisha kumtumia wakala wa benki ili kufanya **malipo ya kodi kwa wakati**, kwa fedha taslimu au kwa njia ya kielektroniki. Takriban nusu ya wanavikundi lengwa vya walipa kodi walipendekeza kubuniwa kwa mfumo wa mtandaoni wa kuomba nambari za udhibiti wa malipo.

Vichocheo vya ulipaji kodi

Walipakodi wanahitaji kuwa na imani na uwezo wa uongozi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuwakamata na **kuwaadhibu wakwepa kodi**; vinginevyo, wanaweza kujihisi vibaya wakati wakwepaji kodi wanapofurahia manufaa lakini hawashiriki mzigo wa kulipa kodi. Washiriki wengi kutoka makundi lengwa ya walipa kodi

waliunga mkono uwepo wa adhabu ya wakwepa kodi, lakini walipendekeza kwamba adhabu yoyote ilingane na kosa, na ianze kwa hatua za kirafiki kabla ya matumizi ya nguvu.

Walipoulizwa jinsi wanavyohudumiwa na uongozi wa mapato ya LGA, wachache walisema walihudumiwa **kwa heshima** huku wengi wao wakiwa na uzoefu mbaya. Ili kuboresha mahusiano na walipa kodi, 42% ya vikundi lengwa vya walipa kodi walipendekeza kuwapa wakusanya mapato mafunzo ya namna bora ya kuwahudumia wateja.

Sheria za kodi zinapaswa kuwa wazi kwa umma ili ziweze kufuatwa. Hata hivyo, wengi wa wanavikundi lengwa vya walipa kodi walionesha wasiwasi wao kwamba sheria na sheria zingine ndogo ndogo hazitangazwi kwa umma mara kwa mara, na kwa wakati. Hii ina maana kwamba walipa kodi wengi wanakuwa hawafahamu mabadiliko katika sheria zinazohusiana na kodi hadi wanapowasiliana na afisa wa usimamizi wa mapato. Walipendekeza kutolewa kwa taarifa za mara kwa mara kuhusu viwango vinavyotumika vya kodi na taratibu za usimamizi ili kuongeza ulipaji wa kodi kwa hiari.

Walipa kodi hawahitaji kufahamu tu nyaraka za kisheria, lakini pia wanahitaji kuelewa maana yake au wakati gani zinapotumika ili kujenga imani na kuuamini mfumo wa kodi. Takriban nusu ya makundi lengwa ya walipa kodi walitaja kuwa hakuna elimu ya walipa kodi ambayo ingewasaidia kuelewa ni lini na jinsi sheria za kodi zinatumika. Wengi walipendekeza kwamba menejimenti za mapato za Serikali za Mitaa ziandae mikutano ya mashauriano ili kuelimisha walipa kodi na kujadili sera za kodi na masuala ya kiutawala, kama vile matumizi ya sheria na kanuni.

Vikundi vyote lengwa vya walipa kodi vinadhani kwa ujumla kwamba **mzigo wa kodi** unaolipwa kwa Halmashauri una changamoto kubwa, hasusan kwa wanaume na wanawake wasio na vyanzo imara vya mapato. Kwa sababu hizo, wengi wao walipendekeza kwamba mamlaka zote za mapato zinahitaji kushirikiana na kuzingatia hali ya mapato ya walipa kodi wanapoweka viwango vya kodi, ada na tozo mbalimbali. Karibu theluthi moja yao pia ilipendekeza matumizi ya malipo kwa awamu.

Takriban nusu ya vikundi lengwa vya walipakodi vilieleza kuwa hawaoni **thamani ya fedha** kwa kulipa kodi, na pia walionesha wasiwasi wao wa kutofahamu jinsi kodi zinavyotumika kwa vile LGA hazitoi taarifa za mapato na matumizi. Wanavikundi wengi walikubaliana kwamba Mamlaka za S/Mitaa zinapaswa kuboresha huduma za kijamii na miundombinu, na theluthi moja ilipendekeza kuboresha mazingira ya biashara ili walipakodi waone thamani ya kodi zao.

Walipoulizwa jinsi watu walio karibu nao wanavyozungumzia kuhusu ukwepaji kodi, nusu ya wajumbe wa makundi lengwa ya walipa kodi walijibu kuwa watu hawajali masuala ya ukwepaji kodi; ni kikundi kimoja tu kati ya vinne ndicho kilieleza kuwa ukwepaji kodi si tabia inayokubalika katika jamii. Wana vikundi wengi walipendekeza kuwa LGA ziweke kipaumbele katika uboreshaji wa huduma za jamii na kueleza vyema jinsi mapato ya umma yanavyotumika ili kubadili mitazamo ya walipakodi kuhusu ukwepaji kodi.

Hitimisho na Mapendekezo

Swali kwamba "nini kinachochea ulipaji kodi kwa hiyari katika ngazi ya serikali za mitaa?" linahitaji majibu mengi kwa kuwa menejimenti za mapato ya Mamlaka za S/Mitaa zinafanya kazi katika muktadha tofauti na kwenye shughuli mbalimbali za kiuchumi na vyanzo vya mapato. Ingawa baadhi ya vichocheo vya ulipaji kodi viko moja kwa moja katika maeneo yenye ushawishi, kama vile elimu ya walipa kodi au huduma nzuri kwa wateja, vichochezi vingine vya ulipaji vinahitaji kushughulikiwa kupitia mamlaka zingine, kama vile kwenye uboreshaji wa utoaji huduma au sera jumuishi ya mapato ambayo ina mgawanyo sawia wa mzigo wa kodi. Hii ina maanisha kwamba sekta binafsi, Mamlaka za S/Mitaa, wakala wa udhibiti, na washirika wa maendeleo wanahitaji kufanya kazi pamoja ili kukuza uzingatiaji wa kulipa kodi kwa hiari na kufanya mchakato wa kukusanya mapato kuwa wa usawa, ufanisi na endelevu zaidi.

Mapendekezo yafuatayo yanaweza kusaidia mchakato huo.

Rahisisha ulipaji kodi

- Kuanzisha kituo kimoja kitakachotoa huduma zote na mifumo ya usajili wa walipa kodi mtandaoni ambayo itakuwa bure.
- Boresha stakabadhi za kifedha zinazotokana na mashine za kielektroniki za fedha (EFD) ili ziweze kudumu, kwa lengo la kuboresha utunzaji wa kumbukumbu.
- Kusanya mapato kupitia simu za kiganjani kuwezesha malipo kufanyika kwa wakati.

Saidia watu kulipa kodi

- Tangaza sheria mpya za kodi kwa wakati. Chapisha na sambaza sheria hizo kupitia gazeti la serikali, magazeti ya ndani ya nchi, Tovuti za Halmashauri, na mbao za matangazo, na machapisho yake yauzwe kwa wananchi kwa bei nafuu. Anzisha kituo cha kutolea taarifa kwa walipa kodi ambapo walipa kodi watajisomea na kufahamu jinsi mazingira ya kisheria yanavyoweza kuathiri shughuli zao za kibiashara.
- Kuelimisha walipakodi kutekeleza haki na wajibu wao. Tumia vyombo nyenzo za habari kama vile mabango, vipeperushi na magazeti kukuza uelewa wa walipakodi kuhusu sheria. Toa programu za elimu ya hiari zinazoshughulikia uzingatiaji wa taratibu za usimamizi na mahitaji ya kuhifadhi kumbukumbu.
- Kutoa ratiba za awamu za kodi bila riba wala adhabu kwa walipakodi wanaotii.

Jenga ubia na Jamii

- Kujenga na kudumisha mazungumzo kati ya mamlaka ya mapato ya ndani na walipa kodi, hususan wanawake, na watu wanaowaamini ili kubuni mikakati maalum ya kutatua tatizo la kutozingatia ulipaji kodi, ambayo inaweka mizani sawa ya matokeo na kuungwa mkono na jamii.

Kuimarisha mahusiano ya kifedha kati ya walipa kodi na Serikali kama mtoa huduma kwa umma

- Pima na ulinganishe mzigo wa jumla wa walipa kodi na mapato au faida wanazopata kwa ujumla na uandae sera jumuishi ya kodi ambayo inazingatia uwezo wa kulipa kodi.
- Chapisha na jadili ripoti za mapato na matumizi ya fedha na walipa kodi ili kujenga imani na uadilifu kwa mifumo ya usimamizi wa fedha za umma.

Weka vikwazo panapo stahili

- Walipakodi hushindwa kuzingatia majukumu yao ya kulipa kodi kwa sababu tofauti; wengine wanapenda kutii lakini hawafanikiwi kila wakati, wengine hawataki kuzingatia ulipaji lakini wanafuatiliwa, na wengine wameamua kutotii kabisa.
- Anza na hatua nyepesi kama vile kukumbushia na utoe ushauri iwapo kuna kosa dogo, kisha fanya ziara za kushtukiza ili kuangalia mahitaji ya msingi ya usajili na uhifadhi kumbukumbu, kufanya ukaguzi wa kina, na chukua hatua kali kama vile kufungua mashtaka kwa kesi zenye kiasi kikubwa cha fedha, ukwepaji wa mara kwa mara, au shughuli za kihalifu.
- Weka wazi uwezo wa kukamata na kuwaadhibu wakwepa kodi. Chapisha onyo mapema dhidi ya tabia ya kutotii, eleza mikakati ya utatuzi wa kutozingatia kulipa kodi kupitia mikutano ya wanahabari ya kila mwaka, himiza vyombo vya habari kuripoti mashtaka yaliyofikishwa mahakamani.

Fuatilia na tathmini ufanisi wa mikakati ya suluhisho la ulipaji kodi

- Fuatilia idadi ya walipakodi ambao hawajasajiliwa kwa kulinganisha na idadi ya walipakodi waliosajiliwa kwa kutumia makadirio ya watu wanaofanya kazi.
- Wakati mfumo wa usajili wa walipa kodi wa mtandaoni utakapokuwa tayari, fuatilia idadi ya maombi ya mtandaoni na ulinganishe na idadi ya maombi yanayotumwa nje ya mtandao.
- Fuatilia mgao wa walipakodi wenye stakabadhi za fedha zinazosomeka/zisizosomeka.
- Wakati mfumo wa maombi ya mtandaoni wa nambari za udhibiti wa malipo utakapopatikana, fuatilia idadi ya malipo ya mtandaoni na ulinganishe na idadi ya malipo ya fedha taslimu.

Utangulizi

Katika jitihada za kitaifa za kukusanya rasilimali za ndani, Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs) zinatakiwa kukusanya mapato yatokanayo na uchumi usio rasmi ambao kwa kiasi kikubwa ukusanyaji wa mapato yake haufanyiki kwa ufanisi kutokana na kutokidhi viwango vya kodi. Udhibiti wa vihatarishi vya kutozingatia ulipaji katika ngazi ya serikali za mitaa unatatizwa zaidi na utofauti wa vyanzo vya mapato vya ndani na mazingira tofauti ya walipa kodi. Katika mazingira kama haya, miradi ya utafiti wa uzingatiaji inaweza kusaidia uundaji wa mikakati madhubuti ya kupata suluhisho.

Kwa sababu hiyo, Sikika iliamua kuangalia vichocheo vya ulipaji kodi kwa kukusanya taarifa kutoka kwa walipa kodi wa ndani ili kuisaidia serikali ya mtaa kuweka mikakati mahususi ya kupata suluhisho na kwa njia hiyo kukuza ulipaji kodi kwa hiari na kukusanya mapato. Utafiti ulifanyika kati ya Januari na Februari 2022 katika mikoa 8 yenye uwiano wa kijiografia na ulihusisha vikundi 24 vya walipa kodi vilivyojadili changamoto zilizojitokeza na pia kutoa mapendekezo kwa menejimenti za mapato ya LGA, ili kukuza uzingatiaji wa kulipa kodi na ukusanyaji wa mapato kwa ufanisi.

Vihatarishi vya Ulipaji Kodi

Ukusanyaji wa mapato katika ngazi ya serikali za mitaa una changamoto kutokana na uwepo wa sheria ndogo ndogo nyingi, uhaba wa wafanyakazi na ujuzi, na mifumo duni ya ukusanyaji, lakini mchakato huo pia hauna tija kwa sababu ya walipa kodi kutofuata sheria. Athari za kutozingatia ulipaji kodi huangazia kwenye mchakato mzima wa usimamizi wa mapato, kuanzia usajili wa walipa kodi, ufuasi wao katika uwekaji wa kumbukumbu, na ulipaji wa madeni yao ya kodi kwa wakati. Sekta isiyo rasmi ina wastani wa nguvu kazi ya zaidi ya watu milioni 20. Lakini mwaka 2016/2017, ni walipakodi milioni 1 tu ndio waliosajiliwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Biashara ndogondogo mara nyingi hazisajiliwi kwa sababu wamiliki wao hawafahamu kanuni, au wanafikiri kwamba biashara zao ni ndogo sana. Tangu mwaka 2018, TRA ilisajili wauzaji wadogo, watoa huduma, na wachuuzi (‘machinga’) kwa mauzo ya kila mwaka ya chini ya TZS 4 milioni kwa kutoa vitambulisho vya TZS 20,000 kwa mwaka. Kuanzia Juni 2018 hadi Juni 2020, vitambulisho milioni 1.59 vyenye thamani ya TZS 31.86 bilioni vilisambazwa, lakini mapato haya yaliingia serikali kuu na si kwa Halmashauri zinazotoa huduma na ulinzi kwa uchumi usio rasmi.

Kikwazo kingine katika ukusanyaji wa mapato ya ndani ni ukosefu wa utunzaji wa kutosha wa kumbukumbu za fedha na maarifa ya kukokotoa dhima ya kodi. Utafiti wa mwisho wa kitaifa kuhusu biashara ndogo ndogo na za kati (MSME) 2012 uligundua kuwa wafanyabiashara wengi wadogo (78.4%) wanatumia leja iliyoandikwa kwa mkono. Wengi wao (76.1%) huhifadhi rekodi za kifedha wenyewe kwa usaidizi wa wanafamilia, marafiki, na wafanyikazi, na ni 2.3% tu ndio walioangaliwa au kukaguliwa na mhasibu aliyeidhinishwa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA). Vitendo kama hivyo vinaweza kuibua kutokubaliana kati ya walipa kodi na watozaji juu ya dhima ya kodi iliyotathminiwa. Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alibainisha mwaka 2022 kuwa Halmashauri 43 zilikusanya TZS 9 bilioni kutoka kwenye tozo ya huduma bila kuwa na maelezo ya mauzo kutoka kwenye mashirika, kuthibitisha utoshelezi wa kiasi kilichokusanywa. Gharama kubwa za uzingatiaji wa kulipa kodi pia ni matokeo ya michakato ya malipo ya kodi yasiyostahili. Kuanzishwa kwa Vifaa vya Kielektroniki vya Fedha (EFD) kulikuwa na matokeo chanya katika uzingatiaji wa kulipa kodi, lakini mawasiliano duni ya Mtandao na uelewa mdogo wa mifumo ya malipo ya kielektroniki ni kikwazo kwa matumizi yao.[1] Ushuru mara nyingi hukusanywa katika vituo vya kuuzia na sokoni, huku vizuizi vya barabarani na vituo vya ukaguzi vikitumika kuhimiza uzingatiaji. Kitendo hiki kimekuwa kikilalamikiwa na wakulima na wafanyabiashara kwani mara nyingi husabaisha ucheleweshaji na unyanyasaji.

Kukomesha tabia (dalili) za ukwepaji wa kodi kwa kuwawekea vikwazo wakwepaji kodi kunaweza kuleta matokeo ya muda mfupi, lakini pia kunaweza kusababisha hisia za chuki dhidi ya mfumo wa kodi na kusababisha kutozingatia sheria zaidi. Hivyo basi, **mkakati endelevu wa kukusanya mapato** unahitaji kuchunguza vichocheo vya msingi vya tabia ya uzingatiaji na kuchagua mkakati unaofaa ambao utashughulikia chanzo (sio dalili) za kutofuata sheria.

1 Kessy (2019), Electronic Payment and Revenue Collection in Local Government Authorities in Tanzania: Evidence from Kinondoni Municipality, Tanzanian Economic Review, Vol. 9 No. 2, pp. 89-106.

Vichocheo vya Ulipaji Kodi

Ili kuboresha uzingatiaji wa kulipa kodi na ukusanyaji wa mapato, mamlaka za mapato zinahitaji kuelewa vichocheo na tabia za walipakodi ili kubuni mikakati ya utatuzi inayoendana na hali ilivyo. Siku za nyuma watanzania wengi walikuwa wakisita kulipa kodi kwa sababu wanaziona kuwa ni mzigo, zisizo na haki wala uwazi. Utafiti wa kimataifa wa Afrobarometer (2021, uk. 65f) uligundua kuwa 46% ya waliohojiwa walisema watu "mara nyingi" au "mara zote" hukwepa kulipa kodi, na theluthi mbili (67%) ya waliojibu "wanakubali" au "wanakubali kwa dhati" kwamba serikali inapaswa kuhakikisha wafanyabiashara wadogo na watu wengine wanaofanya kazi katika sekta isiyo rasmi wanalipa kodi kwenye biashara zao. Masanja (2019, uk. 8) anabainisha kuwa mabadiliko ya kudumu ya sheria na kanuni za kodi yanaleta mkanganyiko miongoni mwa wajasiriamali. Kulingana na utafiti wa Afrobarometer (2021), waliohojiwa wengi (65%) waligundua kuwa ni "vigumu" au "vigumu sana" kujua ni kodi na ushuru gani vinahitajika kulipwa. Masanja (2019) pia alibainisha kuwa utitiri wa kodi unaongeza mzigo mkubwa, hivyo kuwafanya wafanyabiashara wadogo na wa kati kukwepa kodi. Utafiti wa Afrobarometer 2021 uligundua kuwa 32.5% ya waliohojiwa wanafikiri kiasi cha kodi ambacho watu wa kawaida nchini Tanzania wanatakiwa kulipa ni "kiasi kikubwa" au "kipo juu sana". Walipakodi pia walikuwa na wasiwasi kuhusu jinsi kodi zinavyotumika kwani asilimia 70 waliripoti kuwa ni vigumu kujua jinsi serikali inavyotumia mapato yaliyokusanywa.

Tatizo la kiutafiti

Ili kutambua uwezo kamili wa vyanzo vya mapato vya Mamlaka ya S/Mitaa, vihatarishi vya ulipaji kodi vinahitaji kufahamika kwa kina. Hili linahitaji uchambuzi wa sheria ndogo zilizopo kwenye LGA ili kubaini vihatarishi vinavyokwamisha ulipaji kodi kama vile kushindwa kusajili, kushindwa kutunza kumbukumbu zinazohalalisha wajibu wa kulipa kodi, na kushindwa kulipa kwa wakati. Ili kushughulikiwa kwa ufanisi, vihatarishi hivi vyaulipaji kodi vinahitaji kugawanywa kulingana na tabia mahususi za walipa kodi na makundi mbalimbali wanayotoka.

Taarifa zilizopo kuhusu vichocheo vya uzingatiaji wa ulipaji kodi kwa hiari zinapatikana tu katika mfumo wa tafiti zenye uwakilishi wa kitaifa ambazo hazielezi ni kwa nini walipakodi wa ndani hawafuati sheria ndogondogo za Mamlaka ya S/Mitaa zinazosimamia mchakato wa kukusanya mapato ya vyanzo vya ndani. Utafiti huu unajaribu kuziba pengo hilo la taarifa kwa kufanya kazi na Mamlaka za S/Mitaa kubaini mapato yatokanayo na vyanzo vyake vya ndani vyenye uwezo mkubwa wa makusanyo na kuwapa maoni yenye kujenga kutoka kwa walipakodi wa ndani. Lengo ni kuelewa vyema kinachochochea mwenendo wa ulipaji na kubuni mikakati ya utatuzi ambayo itakuza tabia ya ulipaji kwa hiari na ukusanyaji endelevu wa mapato kutoka vyanzo vya ndani.

Malengo ya Utafiti

Ili kuhamasisha ukusanyaji mapato ya ndani katika ngazi ya serikali za mitaa, utafiti una malengo yafuatayo:

1. Kutambua vyanzo vya ndani vyenye uwezo mkubwa wa mapato ambavyo vina vihatarishi vya uzingatiaji na vichocheo vya ulipaji kodi kwa hiari ambavyo vinazuia au kuwakatisha tamaa walipa kodi wa ndani, hivyo, kushindwa kutimiza wajibu wao.

2. Kutoa mapendekezo kwa mamlaka za mapato za LGA ili kubuni mikakati madhubuti ya kupata suluhu ambayo inakuza uzingatiaji wa ulipa kodi kwa hiari na kufikia malengo ya ukusanyaji wa vyanzo vyake vya mapato.

Mbinu za Utafiti

Sampuli za Mapato ya Tawala za LGA

Jedwali 1: Orodha ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa zilizotembelewa



Utafiti huo ulifanyika Januari na Februari 2022 na ulijumuisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka mikoa minane yenye uwiano wa kijiografia ikiwa ni pamoja na Dodoma, Iringa, Dar Es Salaam, Lindi, Singida, Mwanza, Kigoma, na Manyara. Miongoni mwa mikoa hii minane, Halmashauri tatu zilichaguliwa kutoka mijini na Halmashauri tano kutoka pembezoni ili kuchangia mabadiliko ya maendeleo ya kiuchumi na msingi wa kodi. Halmashauri za miji ni pamoja na Jiji la Mwanza (CC), Halmashauri ya Manispaa ya Temeke (MC), na Halmashauri ya Mji wa Babati (TC) wakati Halmashauri za Wilaya (DC) ni pamoja na Wilaya za Kasulu, Kilolo, Mpwapwa, Mtama na Singida.

Halmashauri nne za sampuli ni miongoni mwa zilizoonekana kwa CAG (2022) kwa ukusanyaji wa mapato duni (kama vile Halmashauri ya Mtama yenye 51% tu, ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa na nusu nyingine ilikusanya zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa (kama vile CC ya Mwanza yenye 119%). Hii ina maana kwamba, utafiti unajumuisha sampuli sawia za Mamlaka za S/Mitaa zenye ukusanyaji wa mapato dhaifu na zile zenye uthabiti.

Hatua za Utafiti

Katika hatua ya kwanza, timu ya utafiti ilifanya mkutano wa mashauriano kwa kila uongozi wa mapato ya Halmashauri ili kueleza madhumuni ya utafiti na kushawishi umiliki ili kuhakikisha kwamba matokeo ya utafiti hatimaye yatakuza ukusanyaji wa mapato ya ndani. Timu ilitumia dodoso la kimuundo kutafuta taarifa kutoka kwa maafisa wa usimamizi wa mapato ili kubaini vyanzo vyenye uwezo mkubwa wa mapato ambayo hayajakusanywa, kujifunza kuhusu sheria ndogo zinazohusiana na kodi na kubainisha wajibu wa walipa kodi, na kuchagu makundi ya walipa kodi ambayo yanapaswa kushiriki katika mijadala ya vikundi iliyofafanuliwa hapa chini. Wakati wa mkutano huo, timu ya watafiti pia iliuliza kuhusu jinsi idara za ukusanyaji mapato zinavyotekeleza, kufuatilia na kutathmini mikakati yao ya kutatua vihatarishi vinavyotokana na kutozingatia kulipa kodi.

Katika hatua ya pili, mijadala 24 ya vikundi lengwa ilifanyika (3 katika kila Halmashauri 8) na washiriki wapatao 8 hadi 10 wa makundi ya walipakodi kama ilivyoainishwa kwenye vigezo vya uteuzi wa Halmashauri, huku kundi moja lililolengwa katika kila Halmashauri likiwa na wanawake pekee ili kuibua masuala ya jinsia.[2]

2 Jumla ya washiriki ilikuwa 210.

Washiriki walitambuliwa kwa usaidizi wa maofisa watendaji wa kata na vikundi vya kijamii na ufahamu wa wapi wanavikundi vya uwakilishi vya walipakodi vingeweza kupatikana. Vikundi lengwa vilitoa nafasi ya kutosha kwa ajili ya majadiliano na maswali ya wazi kuchunguza a) jinsi washiriki wanavyochukulia suala la usimamizi wa mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani na uwezekano mkubwa wa ukusanyaji, b) vichocheo vya msingi vya tabia ya kuzingatia ulipaji kodi, na c) kutoa mapendekezo ya namna idara za ukusanyaji mapato za LGA zinavyoweza kuimarisha ulipaji kodi kwa hiari.

Washiriki wa vikundi lengwa hawakujadili suala la utii wa kulipa kodi miongoni mwao kwa hofu ya kufuatiliwa. Fomu za ridhaa ziliwahakikishia kutunziana heshima, usiri na faragha. Wakati wa majadiliano, timu ya watafiti iligundua jinsi ambavyo suala la uzingatiaji linavyoungwa mkono na wengi na jinsi lilivyopewa alama ikiwa ni pamoja na vichocheo vyake.

Uchambuzi

Baada ya mijadala ya vikundi lengwa, timu ya watafiti ilitathmini ni maoni gani yanaweza kujumlishwa kwa kutenganisha yale ambayo kikundi kilifikia makubaliano ya wengi na yale ambayo hayakuwa na mashiko au kufikiwa makubaliano. Katika hatua ifuatayo, uchanganuzi wa ubora wa maudhui ulitumika kwa maoni yaliyokubaliwa ya vikundi lengwa ili kutambua dhana au maana ya kawaida ya majibu yenye maneno tofauti yaliyotolewa na vikundi (kwa mfano dhana ya 'kuheshimiwa' na idara ya ukusanyaji kodi inaweza kuelezewa kama *"maafisa wa LGA kutoa huduma bora kwa kutumia lugha yenye staha kwa walipa kodi" au "mamlaka ya mapato kutoa huduma bora kwa wateja"*). Kisha, timu ya watafiti ilichanganua ni mara ngapi dhana hizo ziliibuliwa na makundi lengwa mbalimbali ili kubainisha masuala makuu. Uorodheshaji wa vikundi lengwa vya vihatarishi vya uzingatiaji vinavyohusiana na chanzo mahususi cha mapato) na vichocheo vya uzingatiaji (vinavyohusiana na chanzo chochote cha mapato) pia vililinganishwa katika makundi yote ili kubainisha maeneo ambayo usimamizi wa mapato ya Mamlaka ya S/Mitaa unapaswa kuyapa kipaumbele kupitia mikakati ya kutafuta suluhisho iliyopendekezwa.

Uorodheshaji wa vihatarishi vya uzingatiaji uliofanywa na vikundi lengwa (vinavyohusiana na chanzo mahususi cha mapato) na vichocheo vya uzingatiaji (vinavyohusiana na chanzo chochote cha mapato) pia vililinganishwa katika makundi yote ili kubainisha maeneo ambayo mamlaka za mapato ya Halmashauri zinapaswa kuyapa kipaumbele kupitia mikakati ya utatuzi iliyopendekezwa. Majibu yaliyotolewa na makundi ya wanawake pekee yalilinganishwa na makundi mchanganyiko au vikundi vya wanaume pekee ili kujua kama masuala ya jinsia ni masuala ya kutilia maanani. Mwisho, vichocheo vya uzingatiaji vililinganishwa na kuchanganua masuala ambayo yamejitokeza katika Halmashauri zote nane.

2 The total number of participants was 210.

Matokeo

Makundi ya walipa kodi

Wakati wa mahojiano na hazina za Mamlaka za S/Mitaa, walitakiwa kubainisha chanzo cha ndani ambacho kina uwezekano mkubwa wa mapato ambayo hayajakusanywa kutokana na uzingatiaji mdogo wa kulipa kodi.

Halmashauri mbili kati ya nane zilizofanyiwa sampuli, Babati TC na Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, ziliona 'tozo ya hoteli' kuwa chanzo kitakachonufaika zaidi kutokana na uelewa bora wa vichocheo vya uzingatiaji kulipaji kodi. Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu na Mtama zote zilichagua ushuru wa mazao ya misitu, huku Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa ikichagua 'ada ya soko la mifugo'. Manispaa ya Mwanza, na Halmashauri ya Wilaya ya Singida, na Manispaa ya Temeke walisema kuwa utafiti huo ungekuwa na thamani kubwa katika ukusanyaji wa 'ushuru wa huduma', 'ushuru wa bidhaa za kilimo' na 'leseni za biashara'.

Jedwali 2: Vyanzo vya Mapato Yasiyokusanywa na Vigezo vya Mgawanyo wa Makundi ya Walipa Kodi

S/N	Wilaya	Chanzo cha Mapato	Vigezo vya Mgawanyo wa Walipa Kodi
1	Babati TC	Tozo za hotelli	Malipo ya hoteli kwa kila chumba (kidogo, cha kati, kikubwa)
2	Kasulu DC	Ushuru wa bidhaa za misitu	Wamiliki wa biashara wenye uzoefu
3	Kilolo DC	Tozo za hoteli	Maeneo yenye watu wengi
4	Mpwapwa DC	Ushuru wa soko la mifugo	Wamiliki wa biashara wenye uzoefu
5	Mtama DC	Ushuru wa bidhaa za misitu	Watoza ushuru wadogo katika maeneo ya ndanindani/pembezoni, jinsia
6	Mwanza CC	Ushuru wa huduma	Wamiliki wa biashara waliosajiliwa, jinsia
7	Singida DC	Ushuru wa mazao ya kilimo	Ukubwa wa biashara, jinsia
8	Temeke MC	Leseni ya biashara	Walipa kodi wenye uzoefu kutoka nje ya jiji, jinsia

Mgawanyo wa walipa kodi katika vikundi vidogo vilivyo na sifa sawa na za uzingatiaji hurahisisha utambuzi wa vihatarishi vya ufuasi na kubuni mikakati ya utatuzi. Vigezo vya mgawanyo wa makundi lengwa ya walipakodi kwa ajili ya kuchagua washiriki vilitofautiana katika wilaya mbalimbali; baadhi ya Halmashauri zilikuwa zikitafuta taarifa kuhusu tabia za walipakodi kulingana na ukubwa wa biashara zao zikionesha uwezo wao wa kulipa kodi, na mamlaka nyingine zilipendelea taarifa kutoka kwa walipakodi kulingana na umbali wa eneo la makazi yao, zikionesha gharama za ukusanyaji wa mapato; kigezo kingine cha mgawanyo kilikuwa uzoefu wa walipakodi unaoonesha uelewa wao wa mchakato wa usimamizi wa mapato.

Timu ya watafiti ilifanikiwa kupanga vikundi lengwa vya wanawake peke yao kuchunguza masuala ya jinsia katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtama, Jiji la Mwanza, Halmashauri ya Wilaya ya Singida, na Manispaa ya Temeke. Hata hivyo, uanzishwaji wa vikundi lengwa vya wanawake peke yao ulikuwa na changamoto katika Halmashauri zingine nne kutokana na idadi ndogo ya walipakodi wanawake katika maeneo hayo. Hivyo basi, utafiti ulijumuisha vikundi vinne vyenye wanawake peke yao, vinne vikiwa na washiriki wa kiume pekee, na vikundi kumi na viwili vyenye mchanganyiko wa washiriki wa kiume na wa kike.

Majukumu ya mlipa kodi

Katika hatua ya pili, idara za ukusanyaji mapato zilieleza ni wajibu gani walipakodi wanapaswa kuzingatia katika maeneo matatu yenye vihatarishi ambayo ni usajili wa walipakodi, utunzaji wa kumbukumbu na malipo kwa wakati. Mwenendo bora wa ulipaji kodi katika maeneo haya yenye vihatarishi unaweza kupanua wigo wa kodi, kusaidia usimamizi wa mfumo wa ushuru ulio wa haki na usawa, na kuzuia ucheleweshaji au dosari kwenye kodi zinazosababisha upotevu wa mapato.

Usajili wa mlipa kodi

Kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato, 2008, kila mkazi anayefanya biashara anatakiwa kutuma maombi ya nambari ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN). TIN inaweza kusajiliwa mtandaoni na bila malipo kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Hata hivyo, baadhi ya shughuli za biashara zinahitaji walipa kodi pia kutembelea na kujaza fomu ya maombi ya kujiandikisha katika Mamlaka za S/Mtaa (na, wakati mwingine, taasisi zingine za udhibiti) ambapo mchakato wa usajili kwa kawaida hufanyika bila malipo.

Utunzi wa Kumbukumbu

Wajibu mwingine muhimu wa mlipa kodi kutokana na Kanuni ya Kodi ya Mapato ya 2012, (Mashine za Kodi za Kielektroniki) ni kudai na kuhifadhi stakabadhi. Kushindwa kudai na kuhifadhi stakabadhi za fedha ni kosa na kuna adhabu ya mara mbili ya kiasi cha kodi iliyokwepwa. Katika ngazi ya S/Mitaa, walipa kodi mara nyingi wanatakiwa kulipa kodi, ada au ushuru katika nyakati na maeneo mbalimbali - kama vile vituo vya ukaguzi - na kuweka stakabadhi za fedha (na wakati mwingine hati nyingine kama vile leseni, vibali au vitabu vya hesabu) ili kuthibitisha jukumu lao la uzingatiaji wa sheria wa kutunza kumbukumbu. Baadhi ya biashara, kama vile hoteli, zinahitajika kuweka rekodi za kiuhasibu - kama vile vitabu vya usajili wa wageni wa hoteli - ili kubaini ukubwa wa kodi.

Ulipaji kodi kwa wakati

Ushuru unapaswa kulipwa pale unapodaiwa. Sheria ya Ushuru wa Mapato (2008), inabainisha kuwa mtu atakayeshindwa kulipa kodi bila sababu za msingi anatenda kosa na anaweza kutozwa faini au kufungwa. Ili kuepuka adhabu hiyo, walipa kodi wanapaswa kutembelea ofisi ya serikali ambako wanapata nambari ya udhibiti wa malipo kisha wamtumie wakala wa benki kulipa kiasi kinachostahili ama kwa fedha taslimu au kwa njia ya kielektroniki (malipo ya mtandaoni kupitia simu ya kiganjani).

Ufuatiliaji wa vihatarishi vya ulipaji kodi

Mamlaka zote za mapato nane za S/Mitaa zilizofanyiwa utafiti zilisema kuwa zinatumia ‘idadi ya walipakodi waliosajiliwa’ kama kiashirio cha vihatarishi vya uzingatiaji wa kulipa kodi, huku mmoja akisema kwamba pia wanazingatia ‘idadi ya walipakodi ambao hawajasajiliwa’. Mamlaka mbili za mapato kati ya nane za S/Mitaa hupima vihatarishi vya uzingatiaji kwa kupitia kumbukumbu zinazolingana na idadi ya walipakodi wanaoweza kuwasilisha kwa Halmashauri stakabadhi na nyaraka zingine zinazohitajika. Mamlaka nyingi za mapato ya S/Mitaa (6 kati ya 8) hupima vihatarishi vya uzingatiaji; ‘malipo ya kodi kwa wakati’ kwa kufuatilia idadi ya waliokwepa kodi, huku wawili kati yao wakifuatilia mapato yanayokusanywa.

Jedwali 3: Ufuatiliaji wa vihatarishi vya ulipaji kodi

Vihatarishi vya Uzingatiaji	Majukumu ya Mlipa kodi	Viashiria vya uzingatiaji kodi
Usajili wa Mlipa kodi	- Usajili mtandaoni kwa TRA (bure) - Usajili kwenye Halmashauri (sio bure muda wote)	- Idadi ya walipa kodi waliosajiliwa - Idadi ya walipa kodi wasiosajiliwa
Utunzaji wa Nyaraka	- Kudai na kuhifadhi risiti za fedha - Kuweka leseni na vibali - Kutunza kumbukumbu za hesabu	- Idadi ya walipa kodi walio na risiti za kielektroniki na hati zingine zinazohitajika
Malipo kwa wakati	- Pata nambari ya udhibiti wa malipo kutoka kwa ofisi ya serikali ya mtaa - Tumia wakala wa benki kufanya malipo kwa fedha taslimu au kuhamisha kielektroniki	- Idadi ya wanaokwepa kodi - Mapato yaliyokusanywa

Vihatarishi vya Ulipaji Kodi

Uandikishaji walipa kodi

Mfumo wa usimamizi wa mapato ya Mamlaka ya S/Mitaa unapaswa kuweka gharama za uzingatiaji wa kodi za kifedha na zisizo za kifedha katika kiwango cha chini. Walipoulizwa kuhusu changamoto zilizojitokeza wakati wa 'mchakato wa usajili wa walipa kodi', 50% ya makundi lengwa 24 ya walipa kodi yalitaja adha ya taratibu za kiutawala zinazotumia muda mwingi pindi wanapotembelea mamlaka mbalimbali za serikali.

> *"Kuna urasimu katika utoaji wa leseni za biashara. Walipa kodi wanazungushwa bila kupewa maelezo kuhusu hali ya maombi waliyotuma. Wakati fulani huchukua hata miezi miwili."* (Mamlaka ya Jiji la Mwanza)

> *"Ofisi za usajili wa mlipa kodi kijiografia ziko katika maeneo tofauti. Kwa mfano, TRA ipo eneo moja na ofisi za LGA ziko sehemu nyingine tofauti."* (Babati TC)

Hata hivyo, hakuna menejimenti ya mapato ya Mamlaka ya S/Mitaa iliyoainisha matatizo yaliyoletwa na 42% ya makundi lengwa yote 24 kuhusu gharama za moja kwa moja za uzingatiaji kama vile ada (kwa mfano kutafuta kibali).[3]

> *"Ada za usajili za mwaka kwa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania, Mamlaka ya Mapato Tanzania, na kamati za vijiji ni kubwa sana na hulipwa kila mwaka."* (Mtama DC)

Ili kupunguza gharama za kufuatilia usajili wa walipa kodi, asilimia 25 ya makundi lengwa ya walipakodi yalipendekeza menejimenti ya mapato ya S/Mitaa kuanzisha vituo vya kutoa huduma kwenye sehemu moja, 33% ilipendekeza mamlaka za mapato kuwatembelea na kusajili walipa kodi kwenye tovuti yao ya biashara, na 38% ilipendekeza kupunguza gharama za usajili.

Utunzaji wa Kumbukumbu

Walipa kodi wana wajibu wa kuhifadhi kumbukumbu zitakazo ruhusu wasimamizi wa mapato kubainisha mzigo wa kodi. Mifumo hii ya Kuhifadhi kumbukumbu inahitaji kuunganishwa kadiri inavyowezekana na mifumo ya biashara na uhasibu iliyokuwepo hapo awali ili kupunguza gharama za uzingatiaji kwa mlipa kodi. Zaidi ya hayo, mifumo ya Kuhifadhi kumbukumbu lazima ihakikishe kwamba nyaraka ziko salama na zinasomeka ndani ya muda unaotambulika kisheria. Hata hivyo, karibu nusu ya makundi lengwa ya walipa kodi (46%) yalitaja kuwa risiti za fedha zilizochapishwa na Mashine za Kodi za Kielektroniki (EFDs) zinafifia na hazisomeki baada ya siku kadhaa.

> *"Changamoto kuu ni kufifia kwa risiti za EFD na hivyo kutosomeka baada ya siku chache kupita."* (Singida DC)

Wakati mmoja kati ya mamlaka nane za mapato za S/Mitaa ikitaja kuwa walipa kodi wanahitaji uelewa mzuri wa urasimishaji biashara, hakuna hata mmoja wao aliyebainisha changamoto za walipa kodi za uzingatiaji na majukumu ya kuhifadhi kumbukumbu kutokana na kufifia kwa risiti zilizochapishwa kutoka kwenye EFDs.[4] Ili kuboresha ufuasi katika jukumu la kutunza kumbukumbu, 29% ya makundi lengwa ya walipa kodi ilipendekeza kuboresha stakabadhi za kifedha za EFD ili ziendelee kusomeka kwa muda mrefu kama inavyotakiwa kisheria.

---

3 Mpango wa Marekebisho ya Udhibiti wa Mazingira ya Biashara ulipendekeza kwamba taasisi za udhibiti hazipaswi kutumia ada za leseni na malipo kwa lengo la kukusanya mapato bali kufidia gharama zilizotumika kwa kutoa huduma au kwa usimamizi. Mpango, uk. xiii.

4 Kanuni ya Kodi ya Mapato(EFD), 2012, toleo la kwanza, sehemu ya pili, inahitaji kwamba mashine za EFD zitoe risiti ambazo zinadumu kwa muda usiopungua miaka mitano.

Malipo kwa wakati

Walipa kodi pia hukabiliana na gharama za kufuata huduma mara nyingi wanapotembelea ofisi mbalimbali za serikali za mitaa, ili kupata nambari ya udhibiti wa malipo na kisha kutumia wakala wa benki kufanya 'malipo kwa wakati' ya kodi zao ama kwa fedha taslimu au kwa njia ya kielektroniki.

> *"Wafanyabiashara wanapaswa kufunga maduka yao ili kwenda kwenye mamlaka za mapato za LGA kukusanya nambari ya udhibiti na kufanya malipo. Hata hivyo, hii inaweza kuchukua muda mrefu wakati mtandao unapofanya taratibu (bila kasi)."* (Mwanza CC)

Mamlaka mbili kati ya nane za mapato ya S/Mitaa zilionesha faida ya mifumo ya malipo ya kielektroniki, kama vile kutuma fedha kwa njia ya simu au kuhamisha kwenye benki, ili kurahisisha 'malipo ya kodi kwa wakati'. Lakini hakuna hata mmoja wao aliyebainisha kuwa ucheleweshaji wa malipo unasababishwa na changamoto za mtandao zinazokwamisha matumizi ya Vifaa vya Kielektroniki vya kulipia fedha; wasiwasi huu ulitolewa na 33% ya makundi lengwa ya walipa kodi.

> *"Mfumo wa malipo ya fedha kielektroniki wakati mwingine hupungua kasi na kusababisha ucheleweshaji wa malipo usio wa lazima pamoja na upotezaji wa muda na gharama za ziada kati ya walipakodi/wafanyabiashara kwa vile malipo yanafanyika katika ofisi za LGA ambazo ziko mbali na eneo la biashara."* (Mwanza CC)

Ili kupunguza idadi ya ziara zinazochukua muda katika ofisi za serikali za mitaa, 42% ya makundi lengwa ya walipa kodi yalipendekeza kubuniwa kwa mfumo wa mtandaoni wa kuomba nambari za udhibiti wa malipo.



Mpangilio wa Vihatarishi vya Ulipaji Kodi

Vikundi vyote lengwa vya walipakodi viliombwa kuorodesha vihatarishi vitatu vya uzingatiaji ili kuonesha ni vipi vinapaswa kupewa kipaumbele na Mamlaka ya S/Mitaa. Kihatarishi cha juu zaidi cha wastani kilihusishwa na 'malipo kwa wakati unaofaa' (1.9) ikifuatiwa na 'kutunza kumbukumbu' (2.0) na 'usajili wa walipa kodi' (2.2). Hata hivyo, tofauti ya wastani huu ni kubwa (takriban 0.8) ikipendekeza kuwa uchanganuzi huo mtambuka sio jumuishi.

Uchambuzi wa wilaya kwa wilaya unaweza kufichua vipaumbele vilivyo wazi zaidi kwa ajili ya kubuni mikakati ya uzingatiaji wa mlipa kodi kwa Halmashauri mojamoja.

Jedwali 3: Ufuatiliaji wa vihatarishi vya ulipaji kodi

Vihatarishi vya Ulipaji Kodi	Wastani kwa Kiwango
Malipo kwa Wakati	1.9
Utunzaji Kumbukumbu	2.0
Usajili wa Mlipa kodi	2.2

Vichocheo vya Ulipaji Kodi

Jinsi ya kushughulika na wakwepa kodi
Walipakodi wanahitaji kuwa na imani juu ya uwezo wa uongozi wa Mamlaka ya S/Mitaa wa kuwakamata na kuwaadhibu wakwepa kodi; la sivyo, wanaweza kujihisi wanyonge wakati wakwepaji kodi wanapofurahia manufaa lakini hawashiriki kwenye mzigo wa kulipa kodi.

Idara tatu kati ya nane za mapato zilisema kuwa utawala wa sheria na hofu ya vikwazo huzuia walipa kodi kukwepa ushuru. Ili kutekeleza utii wa kulipa kodi, mamlaka za mapato za LGA zilisema kuwa zinafanya ukaguzi, kuwaadhibu wakosaji kwa kutumia adhabu au faini, kutaifisha bidhaa, kufunga biashara zao, kuwakamata au kuwafungulia mashtaka. Idadi kubwa (83%) ya makundi lengwa ya walipakodi inafahamu kuwa mamlaka za mapato ya S/Mitaa hukamata wakwepa kodi kwa njia kama vile za ukaguzi na kuweka vizuizi vya barabarani, na wanaadhibiwa kwa kutozwa faini, kutaifishwa au kufunguliwa mashtaka.

> *"Kwa ujumla, ukwepaji wa kodi ni mdogo sana kwa kuwa wafanyabiashara hupokea stakabadhi za malipo ya ada zenye maelezo ya mahali ilipotoka mizigo na inapokwenda. Hata hivyo, baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu wanatumia stakabadhi zisizokubalika na – mara wanapokamatwa – wanatozwa faini kulingana na wingi wa mizigo yao."*
> (Singida DC)

Hata hivyo, 33% ya makundi lengwa ya walipa kodi yalikuwa na wasiwasi kwamba vikwazo vinavyotumika wakati mwingine havilingani, na 33% ya vikundi ilitaja vitendo vya rushwa.

> *"Maafisa wa ukusanyaji mapato wa Mamlaka za S/Mitaa wakati mwingine hutumia nguvu zisizo na ulazima wakati wa ukaguzi hasa wanapoambatana na mgambo [sungusungu]."*
> (Singida DC)

> *"Kuna rushwa, hasa wakati wa mchakato wa makadirio ya ada au malipo. Walipa kodi hutozwa ada kiwango cha chini bila kupewa risiti. Hivyo, Halmashauri inapoteza mapato."*
> (Mpwapwa DC)

Makundi mengi ya walipa kodi (58%) waliunga mkono adhabu kwa wakwepa kodi. Lakini pia walipendekeza kwamba adhabu yoyote ilingane na kosa kwa kuanzia na hatua rafiki kabla ya kutumia nguvu.



Jinsi ya kuwahudumiwa Walipa Kodi

Inafahamika kwamba mwenendo wa walipa kodi unaweza kuathiriwa na motisha, kama vile adhabu za kisheria, lakini hisia pia zina umuhimu wake. Kwa mfano, walipa kodi wana uwezekano mkubwa wa kukubaliana na maamuzi ya wasimamizi wa mapato ikiwa yatashughulikiwa kwa heshima/staha. Hili linahitaji maafisa wa usimamizi wa mapato kuhakikisha kwamba kila wanapokutana wanaacha historia nzuri. Ushirikishaji katika hatua za awali, mtazamo wa kusaidia, uwezo wa kusikiliza, na maswali ya kutia moyo vyote ni muhimu kuwafanya walipa kodi kuamini kwamba wanathaminiwa. Walipoulizwa jinsi wanavyohudumiwa na mamlaka za mapato ya S/Mitaa, wachache (25%) wa vikundi lengwa walisema walithudumiwa kwa heshima huku wengi (58%) wakiripoti huduma mbaya; maoni ya vikundi vilivyosalia yaligawanyika kuhusiana na suala hilo.

“Maafisa ugani wa LGA wanatoa huduma nzuri na wanatumia lugha ya heshima kwa walipa kodi." (Kasulu DC)

"Kuna huduma duni kwa wateja kama vile matumizi ya lugha chafu, matumizi ya nguvu zisizo za lazima, na kupuuza walipa kodi." (Babati TC)

Mamlaka tatu kati ya nane za mapato ya S/Mitaa zilieleza umuhimu wa kuwa na uhusiano mzuri kati ya uongozi wa mapato na walipakodi, na mmoja wao alieleza kuwa wanatoa hati kwa walipa kodi wazuri. Ili kuboresha utoaji huduma kwa walipa kodi, 42% ya vikundi lengwa vya walipa kodi vilipendekeza kuwapa wakusanya mapato mafunzo ya kuwajali wateja.

Taarifa na Elimu ya Kodi

Uelewa wa Sheria Ndogondogo

Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa yanasimamiwa kupitia Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa na zaidi ya sheria ndogo 2,000 ambazo zimetungwa na Halmashauri tangu mwaka 1984. Sheria hizi za kodi zinapaswa kuwa taarifa za wazi kwa umma ili ziweze kufuatwa. Kauli ya "kutojua sheria sio kisingizio" inahakikisha kwamba upofu wa kukusudia hauwezi kuwa msingi wa kuonewa huruma na pia inaiondolea serikali jukumu lake la kuelimisha jamii juu ya kila kipengele cha sheria. Hata hivyo, wananchi wanaweza tu kubeba jukumu la kujielimisha kuhusu sheria ikiwa imetangazwa ipasavyo. Hiyo ina maana kwamba, masuala yote ya kisheria au kiutawala yanapaswa kutangazwa rasmi baada ya kuidhinishwa.

Hata hivyo, 71% ya makundi lengwa ya walipa kodi ilionesha wasiwasi kwamba miongozo na sheria ndogo hazitangazwi kwa umma kila mara, na kwa wakati. Hii ina maana kwamba walipa kodi wengi hawajui mabadiliko katika sheria zinazohusiana na kodi hadi wanapokutana na afisa wa usimamizi wa mapato.

“Hakuna ushirikishaji wa awali wa taarifa kwa wafanyabiashara zinazohusiana na kodi za uzalishaji wa mkaa au usafirishaji. Taarifa zote hutolewa katika ofisi ya ukusanyaji mapato wakati wa malipo. Kwa mfano, kuna ongezeko la tozo za LGA kwenye mkaa kutoka asilimia 5 ya ada za TFS (12500/- gunia) hadi 20,000/-. Mabadiliko haya hayakuwasilishwa kwa walipa kodi.” (KasuluDC)

Ni moja tu kati ya mamlaka nane za mapato za Halmashauri iliyokiri umuhimu wa sheria ndogo za halmashauri kupatikana kwa umma, lakini hakuna hata mmoja wao aliyetaja jitihada mahususi za kuzisambaza. Idadi kubwa (83%) ya makundi ya walipa kodi walipendekeza menejimenti za mapato ya Halmashauri kutoa taarifa za mara kwa mara kuhusu viwango vinavyotumika vya kodi na taratibu za kiutawala ili kuongeza uzingatiaji wa kulipa kodi kwa hiari miongoni mwa wafanyabiashara na kuongeza mapato ya halmashauri.



Kuelewa Matumizi ya Sheria Ndogondogo

Walipakodi hawahitaji kufahamu tu tangazo la sheria, lakini pia wanahitaji kuelewa maana yake au wakati inatumika ili kujenga imani ya walipa kodi katika mfumo wa kodi.[5] Mamlaka tatu kati ya nane za mapato ya S/Mitaa zilisema kuwa elimu ya mlipa kodi inakuza uzingatiaji wa kulipa kodi, baadhi walisema wanawakumbusha walipakodi kabla ya malipo, na wengine walisema wanaongeza uelewa kupitia matangazo ya umma. Hata hivyo, 42% ya makundi lengwa ya walipa kodi yalisema kwamba hakuna elimu ya walipa kodi ambayo ingewasaidia kuelewa ni lini na jinsi sheria za kodi zinavyotumika.

"Hawatoi elimu kwa walipa kodi hata kidogo." (Babati TC)

Zaidi, wengi (75%) wanapendekeza kwamba menejimenti za mapato za S/Mitaa ziandae mikutano ya mashauriano ili kuwaelimisha walipa kodi na kujadili sera za kodi na masuala ya kiutawala, kama vile matumizi ya sheria na kanuni.

5 Ofisi ya Waziri Mkuu (2018), Mpango wa kudhibiti na kuboresha mazingira ya biashara. Dodoma: Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, uk. 6

Mzigo wa Kulipa Kodi

Kodi, ushuri na ada nyingi huongeza mzigo wa jumla wa kodi ambao unaweza kuzidi uwezo wa walipa kodi kuzilipa. Zaidi, walipa kodi wengi hutegemea mapato ya msimu, kwa hiyo, wanaweza kuwa na matatizo ya kulipa kodi kwa wakati unaofaa. Kwa sababu hiyo, mzigo wa jumla wa ushuru na utaratibu wa malipo ya kodi unahitaji kuzingatia utendaji walipa kodi kifedha. Vikundi vyote (100%) vya walipakodi vinafikiri kwamba mzigo wa jumla wa kodi unaolipwa kwa Halmashauri ni changamoto kubwa, hasa kwa wanaume na wanawake wasio na vyanzo vya uhakika vya mapato.

> *"Kuna mzigo mkubwa wa kodi kwa wafanyabiashara kutokana na aina mbalimbali za kodi na tozo za mazao ya misitu ikiwa ni pamoja na Kodi ya Mapato kwa TRA, kibali cha uvunaji wa misitu cha shilingi 180,000/- kwa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), leseni ya uvunaji wa mazao ya misitu ya shilingi 200,000/- kwa TFS, ada ya uvunaji wa mazao ya misitu ya 500,000/- inayotozwa na mamlaka za vijiji, leseni ya biashara ya 105,000/- kwa Halmashauri, tozo ya huduma ya asilimia 2 ya mapato halisi ya Halmashauri, vibali vya mbao 12500/- kwa TFS), ada ya Halmashauri ya asilimia 5 ya kibali cha mbao kinachotozwa na TFS na 2% ya kibali cha mbao kinachotozwa na Mfuko wa Misitu Tanzania, na kibali cha usafiri cha 15,000-30,000/- kulingana na ukubwa wa lori lilobeba."* (Kasulu DC)

Maenejimenti mbili za mapato kati ya nane za Mamlaka za S/Mitaa zilikiri kuwa kodi, ada na tozo tofauti ambazo walipa kodi wanapaswa kulipa zinalipika, na mamlaka mbili zilisema zinawapa walipa kodi muda na nafuu ya malipo ya awali au kuruhusu malipo kwa awamu. Ili kudhibiti mzigo wa jumla wa kodi, 79% ya makundi lengwa yalipendekeza kwamba mamlaka zote za mapato zinahitaji kushirikiana na kuzingatia hali ya mapato ya walipa kodi wanapoweka viwango vya kodi, ada na tozo mbalimbali. Zaidi ya hayo, 29% ya vikundi vilipendekeza matumizi ya malipo kwa awamu.



Faida ya Kulipa Kodi

Madhumuni ya kimsingi ya kodi ni kuipa serikali mapato ili kuhakikisha utoaji wa huduma bora za umma na miundombinu. Hata hivyo, karibu nusu ya makundi ya walipa kodi (46%) yalieleza kuwa hayapati thamani ya kutosha ya fedha zitokanazo na kodi, na asilimia 38 walionesha wasiwasi wao kutojua jinsi kodi zinavyotumika kwa vile Halmashauri hazitoi taarifa za mapato na matumizi.

> *"Hakuna uwiano mzuri kati ya kiasi cha kodi na tozo wanazotozwa walipakodi na ubora wa huduma zinazotolewa na Halmashauri, hususan miundombinu ya barabara ambayo haipo katika hali nzuri na hivyo kuongeza gharama za usafirishaji kwa wafanyabiashara."* (Singida DC)

Nusu ya wasimamizi wa mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa walisema kuwa utoaji wa bidhaa na huduma za umma kama vile maji, barabara na hospitali huhamasisha wananchi kulipa kodi, na makundi mengi ya walipakodi (88%) yalikubali kwamba Halmashauri inapaswa kuboresha huduma za jamii na miundombinu. Zaidi, 33% ya makundi lengwa ya walipa kodi yalipendekeza kuboresha mazingira ya biashara ili walipa kodi waone thamani ya kodi zao.

Utamaduni wa Kulipa Kodi

Voluntary tax compliance requires that taxpayers be self-motivated to conform with (formal) tax laws and want Kulipa kodi kwa hiari kunahitaji walipa kodi wenyewe kuwa na hamasa ya kufuata sheria (rasmi) za kodi na kutaka kuona zikitekelezwa. Tabia hiyo inaweza kukuzwa kupitia mafunzo ya kijamii - mchakato wa uchunguzi na kupitishwa kwa kanuni za kijamii (zisizo rasmi) ambazo zimeenea katika mazingira ya kijamii ya walipa kodi. Ili kuwepo na ufanisi, kanuni kama hizo za kijamii zinahitaji kuwa wazi, na walipa kodi wanahitaji kuwa karibu na vikundi vya kijamii vinavyofuata kanuni hizi.

Walipoulizwa jinsi ambavyo watu walio karibu nao wanavyozungumza kuhusu ukwepaji kodi, asilimia 50 ya makundi lengwa ya walipakodi yalijibu kuwa watu wanaunga mkono kwa mapana ukwepaji kodi; ni asilimia 25 tu ya makundi hayo ndio walioeleza kuwa ukwepaji kodi si tabia inayokubalika katika jamii.

> *"Ni jambo la kawaida na tunahimizana kutolipa kwa sababu hatuoni faida ya moja kwa moja ya kodi zetu."* (Temeke MC)

> *"Jamii ina mtazamo chanya wa malipo ya kodi. Hakuna anayeunga mkono ukwepaji kodi kwa sababu ya aibu ya kijamii inayohusishwa na kufungwa kwa biashara - mbali na adhabu."* (Mpwapwa DC)

Mamlaka tatu kati ya nane za mapato ya S/Mitaa zilitaja umuhimu wa kujenga utamaduni wa kulipa kodi kwa kuwaeleza wananchi kwa nini kila mtu anatakiwa kulipa kodi, na mamlaka mbili zilisema kuwa zinatumia mkakati huu ili kuhimiza uzingatiaji wa kulipa kodi.

Ingawa inaonekana kuwa elimu ya mlipa kodi na mafunzo ya kijamii yanaweza kubadili mitazamo ya walipa kodi kuhusu ukwepaji kodi, asilimia 58 ya makundi lengwa ya walipakodi yalipendekeza kwamba Mamlaka za S/Mitaa ziweke kipaumbele cha kuboresha huduma za jamii na kueleza vizuri zaidi jinsi mapato ya umma yanavyotumika kubadili mitazamo ya wakwepa kodi.

Mpangilio wa Vichocheo vya Ulipaji Kodi

Vikundi vyote vya walipa kodi viliombwa kuorodhesha vichocheo vya uzingatiaji vilivyojadiliwa ili kuonesha ni kipi kinapaswa kupewa kipaumbele na mamlaka ya S/Mitaa. Kiwango cha juu cha wastani kilipewa 'maelezo ya kodi na elimu ya kodi' (2.3) ili kukuza uelewa na matumizi ya sheria ndogo zinazohusiana na kodi, ikifuatiwa na 'mzigo wa kulipa kodi' na 'manufaa ya kulipa kodi' (3.1) Hii inaweza kumaanisha kwamba walipa kodi hawataki tu kuelewa mfumo wa kodi lakini pia wanataka usawa ulioboreshwa kati ya kile wanachotoa na kile wanachopata kama malipo. Kiwango cha nne cha wastani kilikuwa 'kuhudumia walipa kodi' (3.7) ikifuatiwa na 'utamaduni wa kodi' unaounga mkono ukwepaji kodi (4.3). Nafasi ya mwisho (4.5) ilipewa 'kushughulika na wakwepa kodi'.[6] Hii inaweza kumaanisha kwamba walipa kodi hawaoni umuhimu wa kuweka shinikizo zaidi la kulipa kodi kupitia mamlaka za serikali au jamii huku wakiwa na maswali ya kimsingi kuhusu jinsi gani na kwa nini wanapaswa kutii majukumu ya kulipa kodi.

Jedwali 5: Nafasi ya Vichocheo vya Ufuasi

Kichocheo cha Utii	Kiwango cha Wastani
Taarifa na Elimu ya Kodi	2.3
Mzigo wa Kulipa Kodi	3.1
Faida za Kulipa Kodi	3.1
Uhudumiaji Walipa Kodi	3.7
Desturi ya Ulipaji Kodi	4.3
Kushughulika na Wakwepa Kodi	4.5

6 Mpangilio wa kiwango cha wastani wa kando ulikuwa 1.6.

Uchambuzi wa Jinsia

Mlinganisho wa majibu kutoka kundi la wanawake peke yao na makundi yanayolenga wanaume tu unaonesha kwamba walipa kodi kutoka jinsia zote wana hisia sawa - kwa kiasi kikubwa - kuhusu mfumo wa usimamizi wa kodi wa mamlaka za S/Mitaa. Mlinganisho wa majibu kutoka kundi la wanawake peke yao na vikundi vya wanaume tu, unathibitisha hilo. Hata hivyo, uchambuzi wa jinsia unaonesha kwamba mapendekezo yao wakati mwingine yanatofautiana. Vikundi lengwa vya wanaume vinatilia mkazo zaidi hatua za kuhakikisha haki na usawa kwa walipa kodi inatendeka, huku makundi ya wanawake pekee yakisisitiza kuwa kukosoana kunapaswa kuzingatia heshima zaidi. Makundi ya wanawake pia yalionekana kuwa na shauku zaidi ya kupokea taarifa za kodi kupitia njia mbalimbali, huku makundi ya wanaume yakipendekeza mbinu shirikishi zaidi kama vile mikutano ya hadhara na semina za kupokea elimu ya kodi. Ili kuboresha uwiano kati ya gharama na manufaa ya kodi, mapendekezo ya vikundi vya wanaume yalilenga katika kupunguza mzigo wa kodi kwa ujumla, huku mapendekezo ya makundi ya wanawake yalielekeza kwenye uboreshaji wa utoaji wa huduma za umma.

Hata hivyo, inapaswa kukumbuka kwamba uchanganuzi huu wa kijinsia unatokana na sampuli ndogo ya makundi manne tu ya wanaume na manne ya wanawake. Hivyo basi, matokeo yaliyowasilishwa hayawezi kuchukuliwa kuwa ya mwisho. Utafiti zaidi unahitajika ili kuelewa vyema jinsi wananchi; wanaume na wanawake wanavyoathiriwa na mfumo wa kodi wa Halmashauri.

Majadiliano

Vihatarishi vyaUlipaji kodi

Uchambuzi unaonesha kuwa walipakodi wanakabiliwa na gharama mbalimbali za kifedha na zisizo za kifedha ambazo zinapaswa kupunguzwa kuwa kiwango cha chini ili kukuza uzingatiaji wa kanuni za kodi na ukusanyaji endelevu wa mapato. Ingawa hakuna menejimenti ya mapato ya Mamlaka za S/Mitaa iliyozingatia gharama kubwa za usajili wa walipakodi, baadhi (42%) ya vikundi lengwa waliitaja kama changamoto. Mpango wa Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara (2018) ulitayarishwa ili kushughulikia ombi la sekta binafsi la kuboresha uratibu miongoni mwa taasisi nyingi za udhibiti. Kama ilivyo kwa vikundi lengwa, Mpango huo uliibua wasiwasi kuhusu gharama kubwa za kufuata huduma, na ilipendekeza kwamba taasisi za udhibiti zinapaswa kutenganisha dhana ya mapato kutoka kwa mantiki ya udhibiti na kutoza ada za leseni ili kukidhi gharama ya kutoa huduma au usimamizi.[7] Mpango huu pia uliunga mkono wazo la kuanzisha vituo vya huduma kuwa katika sehemu moja ili kuimarisha uratibu na kupunguza mzigo wa udhibiti kwa sekta binafsi

Hakuna mamlaka za mapato za S/Mitaa zilizobaini changamoto za walipa kodi za kutotii wajibu wa kutunza kumbukumbu kwa sababu ya kutokuwepo kwa stakabadhi zilizochapishwa kwenye Mashine za Kielektroniki za Fedha. Takriban nusu (46%) ya makundi lengwa yalibainisha hili kama changamoto. Kanuni za Kodi ya Mapato za 2012 zinahitaji kwamba EFD zitoe risiti ambazo zinadumu kwa kipindi kisichopungua miaka mitano.[8] Walipa kodi hawafahamu ni nani wa kumwajibisha kutokana na tatizo hili la kiufundi.

Kichocheo kingine chenye gharama zisizo za kifedha ambacho hakikutajwa na mamlaka ya mapato ya Halmashauri ni ziara nyingi zinazochukua muda ambazo walipakodi wanapaswa kuzifanya wanapokwenda katika ofisi mbalimbali za serikali ili kupata nambari ya udhibiti wa malipo. Kwa bahati nzuri, Programu ya Utawala Bora wa Fedha[9] inashirikiana na Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kutengeneza programu kupitia simu za kiganjani ambayo itasaidia ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka za S/Mitaa kielektroniki, hasa kutoka kwa ushuru wa huduma, leseni za vileo na za biashara. Programu hiyo ya kimtandao inatarajiwa kuanza kutumika katika mwaka wa fedha wa 2022/2023.

Vichocheo vya Ulipaji Kodi

Kando na gharama za kifedha na zisizo za kifedha, kikundi kinachoangazia walipa kodi pia kilibainisha mfululizo wa mambo ya kisaikolojia, kijamii na vikwazo ambavyo huathiri tabia ya kuzingatia maagizo ya ulipaji kodi. Mamlaka nyingi za mapato za S/Mitaa na vikundi lengwa vya walipa kodi vilikubaliana kuwa elimu ya kodi ni kichocheo muhimu cha ulipaji kodi. Hata hivyo, makundi lengwa yalielezea hisia zao kwamba hawapewi taarifa za kodi, viwango vinavyotumika na taratibu za usimamizi hadi pale wanapokutana na afisa wa mamlaka ya mapato.

Jambo lingine muhimu ni kwamba vikundi lengwa viliibua suala la kutokuwa na usawa kati ya gharama na faida za kukatwa kodi. Takriban makundi yote yalionesha wasiwasi juu ya mzigo wa jumla wa kodi na wengi walilalamika kuhusu uhaba wa huduma za umma na utoaji wa huduma. **Makundi mengi ya walipa kodi** yalipendekeza kuwa uboreshaji wa utoaji wa huduma za umma unaweza kubadilisha mtazamo wa jamii wa kuwaonea huruma wakwepa kodi.

Wakati makundi mengi ya walipakodi yalionesha kuguswa na huduma duni kwa wateja kwenye baadhi ya S/Mitaa, baadhi ya walikiri kwamba utoaji huduma kwa walipakodi umeboreshwa. Uchambuzi unaonesha kuwa mamlaka nyingi za mapato za S/Mitaa zinazingatia mikakati ya utekelezaji ili kukuza uzingatiaji wa kulipa kodi. Ingawa makundi lengwa ya walipa kodi yanaunga mkono mkakati wa kuwazuia wakwepa kodi, theluthi moja walionesha wasiwasi wao kuhusu adhabu isiyo na uwiano na kupendekeza kuanza kuwachukulia hatua laini na kuchukua hatua kali dhidi ya wale tu ambao wameamua kutotii maagizo ya kulipa kodi.

---

7 Mpango wa Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara (2018), uk. XIII.
8 Sheria ya Kodi ya Mapato (EFD) Kanuni, 2012, Mpango I, sehemu 2, kipengele 5.
9 Programu ya Utawala Bora wa Fedha (GFG) inafadhiliwa na Umoja wa Ulaya, Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (GIZ), na Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi (SDC).

Tathmnini na Ufuatiliaji wa Mikakati ya Vihatarishi vya Ulipaji Kodi

Ili kutathmini ufanisi wa mikakati ya kuondoa vihatarishi vya kutozingatia ulipaji kodi, mamlaka za mapato za S/Mitaa zinahitaji kufuatilia viashiria vya uzingatiaji vinavyofaa. Uchambuzi unaonesha kuwa idara nyingi za ukusanyaji mapato zinazingatia idadi ya walipa kodi waliosajiliwa na wakiukaji. Ni wachache tu wanaoonekana kufahamu idadi ya walipa kodi ambao hawajasajiliwa, hali ambayo inaweza kuibua wasiwasi wa usawa kwa wale wanaobeba mzigo wa kodi. Hakuna mamlaka ya mapato ya Halmashauri inayoonekana kufuatilia idadi ya maombi ya mtandaoni ya usajili wa walipa kodi ili kupunguza gharama za ufuatiliaji.

Makundi mengi ya walipa kodi yanafahamu wajibu wao wa kutunza stakabadhi za fedha, lakini stakabadhi zinafifia haraka kwa sababu za kiufundi. Mamlaka nyingi za mapato za S/Mitaa zinaonekana kutopima uzingatiaji wa walipakodi na wajibu wa kutunza kumbukumbu. Wakati mamlaka zinafuatilia idadi ya waliokwepa kodi, hakuna hata mmoja wao anayeonekana kufuatilia idadi ya malipo ambayo hufanywa kielektroniki ili kupunguza gharama za kufuata huduma.

Hitimisho na Mapendekezo

Swali kwamba "*ni mambo gani yanachochea uzingatiaji wa kulipa kodi kwa hiari katika ngazi ya serikali za mitaa?*" linahitaji majibu mengi kwa kuwa mamlaka za mapato ya S/Mitaa zinafanya kazi katika mazingira tofauti na kwenye shughuli mbalimbali za kiuchumi na pia vyanzo vya mapato. Hata hivyo, utafiti uligundua baadhi ya masuala ambayo yamejitokeza kwenye mamlaka zote za serikali za mitaa zilizofanyiwa utafiti, kama vile gharama kubwa za usajili, kufifia kwa risiti za fedha, na tofauti za taratibu za malipo.

Moja ya matokeo makubwa ni kwamba mamlaka chache za mapato ya S/Mitaa zinaonekana kuwa na uelewa wa kutosha wa kwa nini walipakodi wanashindwa kufuata sheria hizo. Ingawa baadhi ya vichocheo vya kutii kulipa kodi viko katika nyanja zao za ushawishi, kama vile elimu kwa walipa kodi au huduma bora kwa wateja, vichocheo vingine vya kuzingatia vinahitaji kushughulikiwa kupitia mamlaka nyingine, kama vile utoaji wa huduma bora au sera jumuishi ya mapato ambayo inagawa kwa usawa mzigo wa jumla wa kulipa kodi. Hii ina maana kwamba sekta binafsi, Mamlaka za Serikali za Mitaa, wakala wa udhibiti, na washirika wa maendeleo wanahitaji kufanya kazi pamoja ili kukuza uzingatiaji wa kulipa kodi kwa hiari na kufanya mchakato wa kukusanya mapato kuwa wa usawa, ufanisi na endelevu zaidi.

Mapendekezo yafuatayo yanaweza kusaidia mchakato huo.

Rahisisha Ulipaji Kodi

- Anzisha vituo vya kutolea huduma zote katika sehemu moja na mifumo ya bure ya usajili ya walipa kodi mtandaoni.
- Ongeza ubora wa stakabadhi za fedha za EFD zisifutike ili kukuza utunzaji wa kumbukumbu.
- Kusanya mapato zaidi kupitia maombi ya simu za mkononi ili kuwezesha malipo kwa wakati.

Saidia ulipaji kodi

- Tangaza sheria mpya za kodi kwa wakati. Zichapishe na zisambaze kupitia gazeti la serikali, magazeti ya ndani, tovuti ya Halmashauri na mbao za matangazo kwa umma na utoe nakala zilizochapishwa na kuzisambaza kwa umma kwa bei nafuu. Anzisha vituo vya habari vya walipa kodi ambapo walipa kodi wanaweza kupata taarifa kuhusu jinsi mazingira ya kisheria yanavyoathiri shughuli zao za biashara.
- Himiza walipakodi kutekeleza haki na wajibu wao. Tumia nyenzo mbalimbali za habari, kama vile mabango, vipeperushi na magazeti, ili kukuza uelewa wa walipa kodi kisheria. Toa programu za elimu ya hiari zinazoshughulikia uzingatiaji wa taratibu za usimamizi na mahitaji ya kuhifadhi kumbukumbu.
- Toa ratiba sanifu za ulipaji kodi kwa awamu bila riba wala adhabu kwa walipa kodi wanaotii.

Jenga Ubia na Jamii

- Jenga na kudumisha mazungumzo kati ya mamlaka ya mapato ya ndani na walipa kodi, hasa wanawake, na watu wanaowaamini ili kubuni mikakati maalum ya suluhu ya ulipaji kodi ambayo inaweka sawa matokeo ya utii na uungwaji mkono wa jamii.

Imarisha mkataba wa jamii wa kifedha kati ya walipa kodi na Serikali kama mtoa huduma kwa umma

- Pima na ulinganishe mzigo wa jumla wa walipa kodi na mapato au faida yao kwa ujumla na uandae sera jumuishi ya kodi ambayo inazingatia uwezo wa walipa kodi.
- Chapisha na jadili na walipa kodi ripoti za mapato na matumizi ya fedha ili kujenga imani yao katika uadilifu wa mfumo wa usimamizi wa fedha za umma.

Weka vikwazo panapostahili

- Walipakodi hushindwa kuzingatia majukumu yao ya kulipa kodi kwa sababu tofauti: wengine wanataka kutii lakini hawafanikiwi muda wote, wengine hawataki kutii hadi wakifuatiliwa, na wengine wameamua kutotii kabisa. Anza na hatua nyepesi kama vile kukumbusha na utoe ushauri ikiwa kuna dosari ndogo, kisha fanya ziara za kushtukiza ili kuangalia mahitaji ya msingi ya usajili na kuhifadhi kumbukumbu, fanya ukaguzi wa kina, na chukua hatua kali kama vile kufungua mashtaka kwa kesi za kiasi kikubwa, ukwepaji sugu, au shughuli za uhalifu.

- Dhihirisha wazi uwezo wa kukamata na kuwaadhibu wakwepa kodi. Chapisha maonyo mapema kwa wenye tabia ya kutotii, eleza mikakati ya suluhu ya kuzingatia utii katika mikutano ya kila mwaka ya wanahabari, na uhimize vyombo vya habari kuripoti walioshtakiwa.

Kufuatilia na kutathmini ufanisi wa mikakati ya suluhu ya ulipaji kodi

- Fuatilia idadi ya walipakodi ambao hawajasajiliwa kwa kulinganisha na idadi ya walipakodi waliosajiliwa na makadirio ya watu wanaofanya kazi.
- Wakati mfumo wa usajili wa walipa kodi mtandaoni utakapopatikana, fuatilia idadi ya maombi ya mtandaoni na ulinganishe na idadi ya maombi yaliyoletwa mezani.
- Fuatilia mgao wa walipa kodi kwa kuangalia stakabadhi za fedha zinazosomeka/zisizosomeka.
- Wakati mfumo wa maombi ya mtandaoni wa nambari za udhibiti wa malipo utakapokamilika, fuatilia idadi ya malipo ya mtandaoni na ulinganishe na idadi ya malipo ya fedha taslimu.

Mapendekezo kwa ujumla

Anzisha mifumo ya usajili wa walipakodi bila malipo

Kuboresha maisha marefu ya risiti za fedha

Kusanya mapato zaidi kupitia programu za simu za mkononi

Tangaza sheria mpya za kodi kwa wakati

Kuelimisha walipakodi kutekeleza haki na wajibu wao

Toa ratiba sanifu za awamu za kodi

Jenga ushirikiano na jamii

Tengeneza sera jumuishi ya kodi ambayo inazingatia uwezo wa walipa kodi kulipa

Chapisha na kujadili na walipa kodi ripoti za mapato na matumizi ya fedha

Ondoa vikwazo kwa kuweka uwiano

Dhihirisha uwezo wako wa kukamata na kuwaadhibu wakwepa kodi

Fuatilia na kutathmini ufanisi wa mikakati ya uzingatiaji wa kulipa kodi

Orodha ya Rejea

Agricultural Council of Tanzania (2013), Study on Produce Cess Taxation System in Tanzania.

Anuradha, J. (2017), Tax and Gender in Developing Countries: What are the Issues? International Centre for Tax and Development, Summary Brief Number 6.

Financial Sector Deepening Trust (2012), MSME in Tanzania – National Baseline Survey Report.

Fjeldstad, O. H., Katera, L., & Ngalewa, E. (2008), Outsourcing Revenue Collection: Experiences from Local Government Authorities in Tanzania. REPOA Brief.

Fjeldstad, O. H., Katera, L., & Ngalewa, E. (2009), Maybe We Should Pay Taxes After All? – Citizens' Changing Views on Taxation in Tanzania, Research on Poverty Alleviation (REPOA) Special Paper 09.29.

Fjeldstad, O.H., Sjursen, I.H. and Ali, M. (2013). Factors affecting tax compliant attitude in Africa: Evidence from Kenya, Tanzania, Uganda and South Africa.

Forum on Tax Administration Compliance Sub-group (2004), Compliance Risk Management: Managing and Improving Tax Compliance, Organisation for Economic Co-Operation and Development.

Japan International Cooperation Agency (JICA) Japan Development Service Co., Ltd. (JDS) (2016) Country Gender Profile: Tanzania Final Report. Japan International Cooperation Agency (JICA) Japan Development Service Co., Ltd. (JDS).

Kessy, S. S. (2020), Electronic Payment and Revenue Collection in Local Government Authorities in Tanzania: Evidence from Kinondoni Municipality. Tanzania Economic Review, 9(2).

Machogu, C., & Amayi, J. B. (2013), The effect of taxpayer education on voluntary tax compliance, among SMEs in Mwanza City-Tanzania.

Masanja, N.M. ed. (2019), Contemporary Issues in Business. NMM PRINTERS.

Mhagama, H. (2020), Ids Prove Very Useful For Petty Traders-TRA. [online] Dailynews.co.tz. Available at: <https://www.dailynews.co.tz/news/2020-07-135f0c5f77df826.aspx> [Accessed 5 October 2020].

Ministry of Finance and Planning (2016), National Five-Year Development Plan 2016/17-2020/21.

Ministry of Trade and Industry (2012), National Baseline Survey Report – Micro, Small and Medium Enterprises in Tanzania, FSDT.

Mpalanzi, Christian (2012), Business Formalisation in Tanzania -Building a stronger small business sector through formalisation, FSDT Focus Note.

National Audit Office of Tanzania (2020a), Annual General Audit Report on the Audit for Local Government Authorities for the Fiscal Year 2018/2020.

National Audit Office of Tanzania (2020b), Performance Audit Report on Revenue Collection from Own Sources in Local Government Authorities.

National Bureau of Statistics (2019), Tax Statistics Report 2017/18 – Tanzania Mainland.

Olate, C., Orozco, R., Stead, J., Dickinson, B. and Melguizo, A.(2019), What is driving tax morale, OECD.

Price Waterhouse Coopers (2016), Sub-National Public Expenditure and Financial Accountability Assessment in Tanzania.

Prime Minister's Office (2018), Blueprint for regulatory reforms to improve the business environment. Dodoma: Ministry of Industry, Trade and Investment.

Research on Poverty Alleviation (2009), Maybe We Should Pay Taxes After All.

Research on Poverty Alleviation and Michigan State University (2014), Afrobarometer (Round 6) – A comparative series of national public attitude surveys on democracy, markets and civil society in Africa.

Tanzania Revenue Authority (2017), Fifth Corporate Plan. Tanzania Revenue Authority.

World Bank Group (2015), Tanzania economic update: why should Tanzanians pay taxes? The unavoidable need to finance economic development (No. 97720, pp. 1-1), The World Bank.

World Bank Group (2007), Gender and economic growth in Tanzania: Creating opportunities for women. The World Bank.

Zhangazha, T. (2018), Is Machinga Identification Equal To Recognition? [online] Udadisi.org. Available at:
< http://www.udadisi.org/2018/12/is-machinga-identification-equal-to.html?view=sidebar>.

Sikika inafanya kazi ya kuhimiza uboreshaji wa mifumo ya afya na usimamizi wa fedha kupitia uwajibikaji jamii na uraghibishi katika ngazi zote za Serikali

Sikika

Nyumba Na. 1387C
Barabara ya Haile Salassie
Mtaa wa Mwaya, Masaki
S.L.P. 12183, Dar es Salaam, Tanzania.
SIMU: +255 222 26 580 15

Ujumbe mfupi: 0688 493 882
Faksi: +255 22 26 680 15
Barua pepe: info@sikika.or.tz
Tovuti: www.sikika.or.tz
Twitter: @sikika1
Facebook: Sikika1
Instagram: Sikika1
LinkedIn: Sikika Tanzania

Nyumba Na. 340
Mtaa wa Kilimani,
S.L.P 1970 Dodoma,
Tanzania.
Simu: 0262321307
Faksi: 0262321316